# BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA
## MUONGOZO WA USAHIHISHAJI MTIHANI WA
## MTIHANI WA UTAMILIFU KIDATO CHA SITA 2025
## KISWAHILI 2

---

**SEHEMU A (Alama 40)**

1. Mtahiniwa anapaswa kuchambua mitazamo minne (4) inayohusu chimbuko la fasihi kwa kuzingatia udhaifu wa kila mtazamo:

(i) Mtazamo wa kidhanifu – mtazamo huu unadai kuwa fasihi ni zao au kazi ya Mungu na binadamu huiga kazi hiyo.
Udhaifu: Humtenganisha msanii na jamii yake kwa kumfanya ni kama mtu wa ajabu sana.

(ii) Fasihi inatokana na hisi.
Wanadai kuwa lazima pawe na mguso ndipo mwanafasihi aweze kuandika au aeleze jambo Fulani. Kifasihi udhaifu: Fasihi inaweza kuelezea hisi kupitia mtindo wa fasihi lakini fasihi yenyewe si hisi.

(iii) Nadharia ya mwigo
Hii inadai kuwa fasihi imetokana na uigaji.
Udhaifu: Nadharia hii inasisitiza uigaji na kusahau suala la ubunifu wa sanaa katika fasihi

(iv) Fasihi inatokana na sihiri.
Wanadai kuwa fasihi ilichumbuka kama chombo cha sihiri katika kujaribu kuyashinda mazingira.
Udhaifu: Mtazamo huu huchanganya dhima na chimbuko. Kutumika fasihi katika sihiri hakumaanishi ndiyo chimbuko lake.

(v) Mtazamo wa Kiyakinifu.
Wanadai chanzo cha fasihi ni saw ana chanzo cha binadamu mwenyewe. Hubadilika kutokana na mazingira na wakati.
Udhaifu: Mtazamo huu hauna udhaifu wowote na ndio unaoungwa mkono na wataalamu wengi wa fasihi.
**Alama 2 ½ kila kipengele**

2. Mtahiniwa anapaswa kueleza maana ya dhana za kifasihi kama ifuatavyo:

(i) Mizani - Ni idadi ya silabi katika mshororo au mstari mmoja katika ubeti wa shairi. Mf.
" Kama wali umekwisha, nipeni hata ukoko
1 2 3 4 6 6 7 8 1 2 3 4 5 7 7 8

(ii) Urari: Ni ulingano au uwiano wa mizani na vina katika shairi. Mf.
Chawa ukimuona, haraka muweke dole

(iii) Ukwapi: Ni kipande cha kwanza katika mshororo wa shairi. Mf.
Njiwa ameshanitoka, nimpate wapi mwingine?

(iv) Utao: Ni kipande cha pili katika mshororo wa shairi. Mf.
Njiwa ameshanitoka, nipate wapi mwengine?

(v) Mleo: Ni mshororo wa tatu katika ubeti wa shairi. Mf.
……………………., ………………………………..
……………………., ……………………………….,
……………………., ………………………………..
Mke akiwa mbishi, wa kushindana kusema.
**Alama 02 kila kipengele**

3. Mtahiniwa anapaswa kueleza kwa ufupi matumizi hasi ya fasihi.
   (i) Kuibua migogoro katika jamii. Mfano kupitia kejeli, utani na nyimbo za mafumbo.
   (ii) Kudumaza maendeleo katika jamii. Mfano baadhi ya methali hutumika vibaya kama vile haraka haraka haina baraka.
   Aliye juu mngoje chini.

   (iii) Hupelekea mmomonyoko wa maadili katika jamii. Mf. Nyimbo nyingi hasa Bongo Fleva zinaimba na kuchochea ngono.
   (iv) Huchochea wizi/ujambazi katika jamii. Mf. Baadhi ya riwaya huonesha jinsi watu walivyofanikiwa kupitia ujambazi. Mf. Riwaya ya Joka la Mdimu.
   (v) Huchochea mwigo uliohasi kwa jamii. Mf. Tamthiliya zinazoelezea Maisha yasiyo halisi hasa kwenye mapenzi baadhi ya watu hasa vijana hudhani ni Maisha halisi.
   (Na hoja nyingine zinazoendana na swali apewe alama)
   **Alama 02 kila kipengele**

4. Mtahiniwa anapaswa kueleza kwa ufupi mbinu za kifani zilizojitokeza katika Habari aliyopewa.
   (i) Muundo – Mtunzi ametumia muundo wa moja kwa moja kuelezea matukio ya utupaji na mauaji ya Watoto wachanga na mwishowe kuishia kufungwa gerezani.
   (ii) Mtindo – Mtunzi ametumia mtindo wa masimulizi (monolojia) kwa kiasi kikubwa na pia majibizano |(daiolojia) katika sehemu ya mwisho wa matini kati ya Jaji na Chausiku. Matumizi ya nafsi yametumika, pia mtunzi ametumia matumizi ya bango katika kuwasilisha kazi yake.
   (iii) Wahusika – Binadamu wametumika kama vile Chausiku, Jaji Makende, Watoto wachanga, polisi wanawake, watangazaji, Hamida n.k.
   (iv) Mandhari – Mandhari halisi kama vile Kariakoo na mahakamani.
   (v) Matumizi ya lugha
   Lugha nyepesi na fasaha imetumika. Pia matumizi ya tamathali za semi kama vile Tashihisi. Mf. Damu ya mtu huwa inalia

Tashibiha. Mf. Kitoto kilichotupwa jalalani kama takataka.
Wanawake waliandamana kama sisimizi.
Msemo. Wangekiona cha mtema kuni.
**Alama 02 kila kipengele**

**SEHEMU B (Alama 60)**

5. Swali linamtaka mtahiniwa kueleza namna washairi walivyoweza kutumia tamathali za semi katika kazi zao.
   CHUNGU TAMU
   - Tashibiha. Kichwa chake kama kifutu
     Samaki kama maji

   - Sitiari: Ushairi ni sukari tamu, uk. 12
     Utoto ni kito

   - Tabaini: aponya, aua. (Uk. 17)
     Kuwaza na kuwazua (uk. 9)

   - Tashihisi: Kifo kimeniita (uk. 14)
     Huzuni imenisaliti (uk. 10)

   FUNGATE YA UHURU
   - Tashibiha. Mbu ndani kama ndege wa vitani
   - Sitiari. Sasa jamvi la wageni, wajapo huwapokea
   - Tafsida. Paka shume – Mtu mwenye tabia mbaya

   MAPENZI BORA
   - Tashibiha. Chuki ni kama nyamafu ina vundo la harufu
   - Sitiari. Mapenzi kwetu dhahabu tuwe nayo Kiarabu
   - Tashihisi. Tunachekwa na wadudu wajinga wa kuabudu
     Na tamathali za semi nyingine atakazotoa mtahiniwa apewe.

   **Utangulizi: alama 02**
   **Kiini: 02 @ 08 alama 16**
   **Hitimisho: Alama 02**
   **JUMLA Alama 20**

6. Mtahiniwa anapaswa kuelezea kwa kina vilio au makemeo ya washairi juu ya maovu yanayotokea kwenye Maisha yao ya kila siku katika jamii zao.

   CHUNGU TAMU
   - Kupiga vita dhulma - Chaku na kuku
   - Kupiga vita matabaka - Manzese – Ostabei, Punda

- Kupiga vita ubaguzi - Thomas na Dotto
- Kupiga vita usaliti - Chatu na Kuku

KIMBUNGA

- Kupiga vita rushwa - Rushwa
- Kupiga vita umbea - Wacha hayo, Hayafai mtaani
- Kupiga vita wizi - PAKA
- Kupiga vita usaliti - KIBWANGAI
- Kupiga vita ukoloni mamboleo - CHUI

FUNGATE YA UHURU

- Kupiga vita uongozi mbaya - WIZI, FUNGATE YA UHURU
- Kupiga vita ukoloni mamboleo - JOKA LA MDIMU, AFRIKA
- Kupiga vita uvivu - MCHEZA HAWI KIWETE
- Ubadhilifu wa mali za umma - WIZI

MAPENZI BORA

- Kupiga vita choyo - Ubeti 202, 383
- Kupiga vita ubaguzi - Ubeti, 147
- Kupiga vita dhulma - Ubeti 152
- Kupiga vita chuki - Ubeti 333

**Utangulizi - alama 02**
**Kiini - Alama 02 @ 4 x 2 = 16**
**Hitimisho - Alama 02**
**JUMLA ALAMA 20**

7. Swali linamtaka mtahiniwa kuelezea nafasi ya mwanamke katika jamii kwa kutumia tamthiliya mbili kati ya alizozisoma.

NGUZO MAMA

(i) Jasiri na mwenye kujitoa mhanga - Bi Nane
(ii) Chombo cha starehe - Bi Sita
(iii) Viumbe dhaifu wasioweza kufanya chochote - Mwanamke wa Patata
(iv) Kiumbe duni na kisichoweza kufanya maamuzi – Bi Saba na Bi Pili

MORANI

(i) Mwanamapinduzi - Jalia
(ii) Chombo cha Starehe - Aisha
(iii) Jasiri - Jalia
(iv) Kiumbe duni na mlevi - Aisha

KIVULI KINAISHI

(i) Kiongozi mbaya - Bi Kinimbwe
(ii) Mchawi - Bi Kinimbwe

(iii) Mwenye upendo - Bibi Kizee
(iv) Mwanamapinduzi - Bibi Kizee

KWENYE UKINGO WA THIM

(i) Mwanamapinduzi - Martha
(ii) Mwenye kunyanyaswa - Martha
(iii) Mwenye kudhulumiwa - Martha
Na nafasi nyingine za mwanamke

**Utangulizi - Alama 02**
**Kiini - 02 @ 08 alama 16**
**Hitimisho - Alama 02**
**JUMLA ALAMA 20**

8. Mtahiniwa anapaswa kuonyesha mchango wa vijana katika jamii zao kwa kutumia riwaya mbili alizosoma.

Utangulizi
Aelezee maana ya mchango wa vijana au mchango na maelezo mafupi juu ya mchanfgo wa vijana.

VUTA N'KUVUTE

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | Kupiga vita mila potofu na kandamizi | - | Yasmini |
| (ii) | Kupiga vita ukoloni na unyonyaji | - | Denge na wenzake |
| (iii) | Kupita vita usaliti | - | Denge na wenzake dhidi ya Koplo Matata |
| (iv) | Kuhimiza umoja na mshikamano katika jamii | - | Denge na wenzake |

MFADHILI

(i) Kujitolea kwa kusomesha wahitaji – Gadibullah
(ii) Kufanya kazi kwa bidi kwa maendeleo ya taifa – Gadibullah, Dania
(iii) Kuhamasisha umoja na mshiakamano – Nunu & Boaz
(iv) Kuokoa Maisha ya watu kwa kuchangia damu au kutoa moja ya kiungo cha mwili- Ghadibullah

KUFIKIRIKA

(i) Uongozi bora - Mfalme
(ii) Bidii katika kazi - Utu busara ujinga hasara
(iii) Upendo na usikivu - Mwanri

USIKU UTAKAPOKWISHA

(i) Bidii na kujituma - Chioko
(ii) Mapenzi ya kweli kwa jamii yake, Gonza
(iii) Kupambana na uhujumu Uchumi – Gonza na Chioko
Na michango mingine

| | | |
|---|---|---|
| **Utangulizi** | **-** | **Alama 02** |
| **Kiini** | **-** | **02 @ 08 ALAMA 16** |
| **Hitimisho** | **-** | **Alama 02** |

**JUMLA ALAMA 20**

*Wabillah Tawfiiq*